



PENDEKEZO LA KUONGEZA 40% YA BEI ZA HUDUMA YA UMEME

MIKUTANO YA KUPATA MAONI KUHUSU MAOMBI YA SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) YA KUONGEZA BEI ZA HUDUMA YA UMEME

TAREHE: KATI YA TAREHE 15 NA 22 NOVEMBA 2007

MAHALI: DAR ES SALAAM, ARUSHA, MWANZA, DODOMA
AND MBEYA

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (yaani *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA)*), imepokea maombi ya **Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO)** yenye kumbukumbu Nambari-TR-E-07-012 ya kutaka kuongeza bei zake (*tariff*) za huduma za umeme kwa asilimia 40 (40%).

Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(b) cha Sheria ya EWURA, EWURA itafanya mikutano ya kupata maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi kutoka kwa wadau wa mwombaji ili kujua uhalali wa maombi hayo ya kupandisha bei ya huduma za Umeme.

EWURA imeandaa mikutano itakaofanyika **Dar Es salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma and Mbeya** kati ya tarehe 15 na 22 ya mwezi wa November, 2007, ili kupata maoni ya wananchi, Baraza la wawakilishi wa watumiaji wa huduma za umeme (yaani **Consumer Consultative Council (CCC)**) pamoja na wadau wengine kuhusu ombi hilo la **TANESCO**. Wawakilishi wa **Menejimenti ya TANESCO** pia wamealikwa kwenye mikutano hiyo ili washiriki kwenye taftishi/uchunguzi huu. Tarehe za mikutano hiyo, muda na mahali itakapofanyika mtajulishwa.

Wananchi wote wanaalikwa kuhudhuria. Wale watakaoamua kushiriki kwa kutoa mada yao siku ya taftishi/uchunguzi watatakiwa kujisajili, kupata nakala ya hoja za **TANESCO** na kuwasilisha hoja zao kwa maandishi kabla ya saa 11 jioni mnamo tarehe **5 Novemba, 2007 (Jumatatu)**. Mshiriki atatakiwa kuchangia gharama za kudurufu makabrasha na kuyasafirisha.

Wadau wengine ambao wanapenda kutoa maoni kuhusiana na taftishi/uchunguzi huu wanakaribishwa kuleta maoni yao ki-maandishi na kuyafikisha kwenye anuani iliyoonyeshwa hapa chini, kabla ya tarehe **6 Desemba, 2007 (Alhamisi)**.

***Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Udhubiti wa huduma za Nishati na Maji (EWURA) Ghorofa ya 6, Harbourview Towers (zamani JM Mall Building), Samora Avenue, P O Box 72175, DAR ES SALAAM
Tel: 022 2123850/3/4/6, Fax: 022 2123180,
e-mail:info@ewura.com***